# Zaburi 125

*Siku ya Mungu ya 30/B*

**Gauthier KM**




1. Bwana alipowarudisha wafungwa Sioni,
   tulikuwa kama waota ndoto
   Hapo kinywa chetu kilijaa kicheko.
   na ulimi wetu shangilio.

2. Hapo walisema kati ya mataifa;
   Bwana amewatendea makubwa
   Bwana ametutendea makubwa,
   Tumeona furaha.

3. Uwarudishe, ee Bwana, wafungwa wetu,
   kama mito jangwani mwa kusini .
   Wanaopanda mbegu wakilia machozi ,
   watavuna kwa shangwe

4. Kwenda wanakwenda kwa kulia,
   wakichukua mbegu zakupanda;
   kurudi wanarudi kwa shangwe
   wakichukua miganda yao.